



WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MoEST Weekly

27, Oktoba 2026



**SERIKALI YAWEKEZA BILIONI 60 KUIMARISHA
MAFUNZO YA WATAALAMU WA ANGA
NCHINI**

SERIKALI YAWEKEZA BILIONI 60 KUIMARISHA MAFUNZO YA WATAALAMU WA ANGA NCHINI

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewekeza takribani shilingi bilioni 60 katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kupitia Mradi wa EASTRIP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya wataalamu wa anga na usafirishaji, kuongeza upatikanaji wa wataalamu wenye ujuzi nchini na kupunguza utegemezi wa mafunzo yanayotolewa nje ya nchi.

Uwekezaji huo umekiwezesha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuwa Kituo cha Umahiri cha Kikanda katika Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji (CoEATO), kupitia ujenzi wa miundombinu ya kisasa, uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na kujifunzia, pamoja na kuimarisha uwezo wa chuo kutoa mafunzo ya urubani, uhandisi wa matengenezo ya ndege na wahudumu wa ndani ya ndege (cabin crew), yanayokidhi mahitaji ya soko la ajira katika sekta ya usafiri wa anga.

Miundombinu iliyokamilika inajumuisha majengo matatu ya mafunzo ya anga yenye maabara 15 na karakana tano za kisasa, vyumba 10 vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 512 kwa wakati mmoja, ofisi 13 za wafanyakazi na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 300. Aidha, mradi umewezesha ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,504, yakiwemo nafasi 752 kwa wanafunzi wa kike na 752 kwa wanafunzi wa kiume.

Akizungumzia mafanikio ya uwekezaji huo, Oktoba 26, 2026 Jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Mradi wa EASTRIP katika NIT, Dkt. Chacha Ryoba, amesema uwekezaji huo umeimarisha uwezo wa chuo kutoa mafunzo ya kitaalamu katika fani za anga, ikiwemo urubani, uhandisi wa matengenezo ya ndege, uendeshaji wa shughuli za ndege na huduma kwa abiria ndani ya ndege.

Ameeleza kuwa, pamoja na miundombinu, mradi umewezesha ununuzi wa vifaa maalumu vya mafunzo, vikiwemo vifaa vya kuigiza mazingira ya ndani ya ndege kwa wahudumu wa ndege (cabin crew mock-ups), vifaa vya mafunzo ya matengenezo ya ndege kwa njia ya uhalisia pepe (Virtual Maintenance Trainer), vifaa vya kufundishia mifumo ya ndege na programu za mafunzo kwa njia ya kompyuta. Vifaa hivyo vinaimarisha mafunzo kwa vitendo na kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi unaohitajika katika mazingira halisi ya kazi.



Katika kuimarisha ubora wa mafunzo, NIT imepata utambuzi na ithibati mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Chuo kimetambuliwa kama Shirika la Mafunzo Lililoidhinishwa (Approved Training Organization-ATO) kwa mafunzo ya urubani, uhandisi wa matengenezo ya ndege, maafisa wa uendeshaji wa safari za ndege na kozi za utoaji leseni kwa wahudumu wa ndege. Aidha, chuo kinatambuliwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (IATA) na Shirika la Usalama wa Usafiri wa Anga la Ulaya (EASA), ikiwemo kuwa kituo cha mitihani ya leseni ya uhandisi wa matengenezo ya ndege ya EASA Part-66 na taasisi ya mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege ya EASA Part-147.

Mafanikio hayo yanaongeza fursa kwa Watanzania kupata mafunzo yenye ubora wa kimataifa nchini, huku yakichangia kupunguza gharama za kusomesha wataalamu nje ya nchi na kuimarisha upatikanaji wa wataalamu wenye sifa zinazokubalika katika soko la ajira la ndani na la kimataifa.

Kwa upande wa maendeleo ya kitaaluma, NIT imeendelea kuimarisha programu zake za mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya sekta ya usafiri wa anga na usafirishaji. Aidha, chuo kimeendelea kujenga uwezo wa wakufunzi na watumishi kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi, pamoja na fursa za kujifunza katika mazingira ya kazi ili kuimarisha ujuzi na kuendana na maendeleo ya teknolojia. Mafanikio hayo yanajumuisha marubani watano, wataalamu 10 wa uhandisi wa matengenezo ya ndege wanaopatiwa mafunzo ya leseni, watumishi 18 wanaosoma shahada za uzamili na wataalamu wawili waliopata mafunzo ya tiba ya msingi ya anga. Hatua hizi zinachangia kuongeza weledi wa watumishi na kuboresha ubora wa mafunzo yanayotolewa chuoni.

Uwekezaji huo pia umechangia kuongeza uwezo wa NIT kutoa mafunzo ya elimu ya juu na ya kitaalamu, sambamba na kuimarisha mazingira ya wanafunzi kupata maarifa na ujuzi unaohitajika katika sekta za usafiri wa anga na usafirishaji. Hali hiyo ina umuhimu mkubwa katika kukidhi mahitaji ya mashirika ya ndege, kampuni za matengenezo ya ndege na taasisi nyingine zinazohudumia sekta ya anga.

Kwa ujumla, utekelezaji wa Mradi wa EASTRIP katika NIT unaonesha dhamira ya Serikali ya kuimarisha elimu na mafunzo ya ufundi na ufundi stadi, kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa wataalamu wa anga, kuongeza fursa za ajira kwa vijana na kupunguza utegemezi wa mafunzo ya gharama kubwa nje ya nchi. Uwekezaji huu ni hatua muhimu katika kuimarisha uwezo wa Tanzania kuzalisha wataalamu wenye ujuzi unaokidhi mahitaji ya sekta ya usafiri wa anga na kuchangia maendeleo ya uchumi wa taifa.

